JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA
Tovuti: www.hlpc.go.tz
Simu: 0750059900 Barua Pepe:hlpc@afya.go.tz

# TANGAZO

## KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI APRILI 2026

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa Shahada ya Maabara ya Afya ya Binadamu kuwa dirisha la maombi ya utarajali litafunguliwa tarehe **20.03.2026** Saa **4:00 Asubuhi** na kufungwa **22.03.2026 Saa 9:30 Alasiri.** Hivyo kila mhitimu anasisitizwa kufanya maombi usajili wa awali (provision) ili kumwezesha kufanya maombi ya utarajali. Aidha, Maombi yatafanyika kupitia mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***

**Mambo muhimu ya kuzingatia;**

1. Wahitimu wanaoruhusiwa kufanya maombi ya utarajali ni wale walioomba usajili wa awali baada ya kupata barua ya utambulisho kutoka chuoni (waliosoma nchini)
2. Wahitimu wote waliosoma nje wanatakiwa kuhakikisha wameambatanisha cheti cha uthibitisho kutoka TCU pamoja na cheti cha matokeo au cheti cha taaluma kutoka chuoni
3. Waombaji wote wanatakiwa wawe wamefanya maombi ya usajili wa awali (Provisional Registration) na awe amepata ujumbe (notification) angalau **yamethibitishwa** (***APPROVED).***
4. Waombaji wote wanasistizwa kufanya maombi kwa wakati na ikitokea mwombaji atahitaji kubadili kituo cha utarajali, anaweza hivyo kuhamia kituo chenye nafasi kupitia akaunti ya mwombaji ya mfumo wa hprs.moh.go.tz kabla dirisha halijafungwa. Baada ya dirisha kufungwa mwombaji wa utarajali HAKUTAKUWEPO NA UWEZEKANO wa kubadili kituo cha utarajali.

Aidha; Wale wote watakaochagua vituo vya utarajali wanatakiwa kufika Dodoma Ofisi ya Msajili, Baraza la Wataalam wa Maabara tarehe 27.03.2026 Saa 2:00 asubuhi ili kupatiwa maelekezo pamoja na kupatiwa barua.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
09.03.2026

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
09 MAR 2026
P.O.Box 743
DODOMA